# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA MGENI RASMI, NDG. KHAMIS ABDULLA SAID, KATIBU MKUU **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** KATIKA UFUNGAJI WA MKUTANO WA NANE WA TATHMINI YA PAMOJA YA MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU ZANZIBAR

**UKUMBI WA** MADINATUL BAHRI HOTEL **– ZANZIBAR**
**JUMATANO, TAREHE 11 JUNI 2025**

**KAULI MBIU: MABADILIKO YA ELIMU KWA MUSTAKABALI ENDELEVU KUPITIA UJUMISHI , TEKNOLOJIA NA USTAHAMILIVU**

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Baraza la Wawakilishi, Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi**
**Manaibu Katibu Wakuu; Utawala na Taaluma wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,**
**Mwakilishi wa Katibu Mkuu , Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia**
**Mwenyekiti wa Washirika wa Maendeleo**
**Mfadhili wa Mkutano , WB**
**Wakuu wa Vyuo Vikuu na watendaji wa elimu ya juu**
**Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,**
**Viongozi Wastaafu**
**Wakurugenzi na Watendaji wote wa WEMA Pamoja na maafisa elimu mkoa na wilaya**
**Wawakilishi wa Asasi za Kiraia,**
**Wadau wa Elimu wa Sekta Binafsi**
**Wawakilishi wa Skuli binafsi**
**Wazazi, Walezi, Walimu na Wanafunzi**
**Wanahabari**
**Wageni waalikwa**
**Mabibi na mabwana**
**Assalam Alaykum Warahmatullah wabarakatu**
**Habari za mchana**

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa afya na kutuwezesha kukamilisha siku tatu za mkutano huu muhimu kwa mafanikio makubwa. Nimefarijika sana kushiriki nanyi leo katika kufunga rasmi Mkutano wa Nane wa Tathmini ya Pamoja ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu Zanzibar.

Pili, binafsi nina furaha kubwa kuungana nanyi leo hii nikiwa kama mgeni rasmi katika ufungaji wa mkutano huu wa nane wa pamoja wa kutathmini maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa mwaka huu 2025. Jukwaa hili ni fursa ya kipekee kwa wadau wote wa elimu kujadili tathmini ya mafanikio na changamoto za sekta ya elimu na kupanga kwa pamoja mikakati madhubuti kwa ajili ya muendelezo wa safari ya mageuzi makubwa ya elimu.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Nachukuwa fursa hii adhimu kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) kuwashukuru washiriki wote kwa kuona umuhimu wa kuhudhuria mkutano huu kwa lengo la kutuunga mkono katika safari yetu ya mageuzi ya elimu.

Shukrani zetu za dhati ziende kwa World Bank (WB) pamoja na washirika wengine kwa kufadhili mkutano huu wa tathimini ya pamoja ya sekta ya elimu ambao sasa tunaufanya kwa mwaka wa nane mfululizo tangu tulipoanza mwaka 2018. Niwaombe wahisani wengine wajitokeze katika kusaidia maandalizi ya mikutano hii ili iendelee kuwa endelevu na sote tunaona umuhimu wake. Aidha, niishukuru kamati ya maandalizi ya mkutano huu kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kukamilisha mkutano huu ambapo

matumizi ya teknolojia yameimarika zaidi. Hongereni sana wote mlioshiriki kwa njia moja au nyengine kuandaa mkutano huu.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Nichukuwe fursa hii pia kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wetu mpendwa wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kuwashukuru Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Raisi -Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na tunashukuru kwa kuleta wawakilishi ambao wamewasilisha mada, kubadlishana uzoefu na kuonesha matendo mazuri.

Pia napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa washirika wetu wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia (World Bank), UNICEF, UNESCO, GPE, KOICA, SIDA, African Development Bank pamoja na wadau wa elimu Goodneighbours, Milele Zanzibar Foundation, Madrasa Early Childhood Program Zanzibar (MECPZ), Mwanamke Initiative Foundation, Shule Direct, SAZANI, RELI Tanzania, Room to Read, KTO, Norwegian Association of Disability (NAD),Green light Foundation, Zanzibar Private School Association, ZAFAYCO, ZAYEDESA kwa kushiriki kikamilifu katika mkutano huu vile vile kwa kutuunga mkono katika miradi ya maendeleo ya sekta ya elimu. Pia napenda kuwashukuru taasisi zetu za serikali Kwarara Media Education Cente (KMEC) na SUZA TV kwa kuturusha mubashara na kutufanya tusikike mbali. Ninapenda kuwashuku walimu na wanafunzi walioleta maonesho yao kutoka Skuli ya Kiswandui, Jango'mbe, Lumumba, Feza, Tumekuja, Mwanakwerekwe Vocational Training Centre, na KIST.

Aidha ninapenda kuwakumbusha kufanya kazi kwa pamoja badala ya kila taasisi kufanya kazi peke yake. *Tukubali kuwa kwa mshikamano na*

*uwajibikaji, elimu bora inawezekana. Tuendelee kushirikiana kubadili ndoto kuwa matendo*. Aidha tunawashukuru wageni wote mlioshiriki mkutano huu kutoka taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

**Kauli mbiu ya mwaka huu na mwelekeo wa mageuzi** ilikuwa inasema: ”Transforming Education for Sustainable Future: Inclusivity, Technology and Resilience” ambayo tumeitafsiri kama Mabadiliko Ya Elimu Kwa Mustakabali Endelevu Kupitia Ujumishi , Teknolojia Na Ustahamilivu

ni wito kwa kila mmoja wetu kutafakari nafasi yetu katika kujenga mfumo wa elimu unaoandaa vijana kwa dunia inayobadilika kwa kasi. Leo, hatuhitaji tu elimu, bali elimu inayoandaa kwa maisha ya sasa na maisha yajayo inayokupa stadi za maisha kama vile fikra tunduizi, ujuzi wa kidijitali, ujasiriamali, ubunifu na uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea. Mtakubaliana nami kuwa elimu isiyokuandaa kwa maisha ya sasa na kesho, si zawadi bali mzigo.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Kauli mbiu yetu inaakisi azma na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT). Serikali zote mbili zina endelea kutekeleza mageuzi makubwa ya elimu nchini ambayo yanawalenga walimu na wanafunzi ili tuweze kupata elimu inayoakisi kasi ya mabadiliko ya karne ya 21.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Nimenong'onezwa kuwa mara hii mkutano ulikuwa na vionjo vya aina yake ambavyo vimesisimua waliohudhuria. Tumeona kwa macho yetu jinsi maonyesho ya wanafunzi, simulizi zao za ushindi za vijana wetu wa walioshiriki mashindano ya Hisabati na Sayansi, walioonesha ubunifu wao na kuwasilisha mawazo yao katika hadhira hii pamoja na mijadala ya wataalamu na wadau, yameonesha dira mpya ya elimu inayoibua vipaji na kupambana na changamoto za karne ya 21. Nimeambiwa kuwa maonyesho ya kazi za ubunifu za wanafunzi zilikuwa nzuri sana sana sana na zimeonesha vipaji vya watoto wetu. Naomba **Tuwapongeze**

Ninaahidi kuwa tutahakikisha kuwa tunaweka miongozo na mikakati ya kuibua na kuendeleza vipaji katika ngazi zote za elimu. Pia nimeambiwa mmepata fursa ya kusikiliza simulizi za wanafunzi walioshiriki mashindano ya Hisabati na Sayansi, kutuwakilisha vyema kwenye medani ya kimataifa na mmepata fursa ya kuonana nao na kuwasikiliza. Niwapongeze wanajeshi hawa wa Dkt Hussein Mwinyi ambao wanaendelea kutusaidia kutafsiri mageuzi ya elimu tunayoyataka kwa vitendo.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua mchango wa elimu katika maendeleo ya taifa na katika kukabiliana na ushindani wa kimaendeleo wa kitaifa na kimataifa. Kwa kulitambua hilo Serikali inaendelea kuwekeza maradufu katika elimu, bajeti ya elimu imeongezeka mara nne. Serikali imeendelea kuweka mikakati madhubuti kwa kushirikiana na wadau wote wa elimu katika kutekeleza malengo yake iliyojiwekea ili kufikia Dira ya

Maendeleo ya Zanzibar 2050 na malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030 hasa elimu yenye ubora wa juu kabisa. Mwenye macho haambiwi tazama. Tumpongeze Jemedari wetu Dr Hussein Ali Mwinyi.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Dhamira ya Serikali ya Awamu ya nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi ni kuimarisha ubora wa elimu ndio maana imewekeza nguvu zote kwenye kuleta mabadiliko ya uchumi wa Zanzibar kupitia utoaji wa elimu bora ambayo utatupatia vijana wa kizanzibari kupambana na mabadiliko ya ulimwengu hasa ya kiteknolojia. Aidha Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amekuwa akisisitiza umuhimu wa mashirikiano na wadau kwa kila sekta ili kusikiliza changamoto zao na kujadiliana mikakati ya kuzipatia ufumbuzi. Tujipongeze kwa kutimiza azma hii.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Nina imani kuwa wadau tumezitumia vizuri siku zote tatu za mkutano huu kujuana, kuanzisha mahusiano mapya ya kikazi, kujadili, kutoa michango na kushauri namna ya kuleta mageuzi ya elimu hapa Zanzibar. Hapana shaka matokeo ya mkutano huu yataongeza kasi kwa kila mdau wa elimu kuchangia kwa nafasi yake kuchochea kasi ya mageuzi ya elimu. Tunatarajia maoni yenu yatakuwa chachu ya mabadiliko katika elimu ya Zanzibar katika ngazi zote kuanzia maandalizi hadi elimu ya juu .

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Matokeo ya mijadali yenu yameonesha umuhimu wa kuwa na mtaala unaolingana na mahitaji ya soko na maendeleo ya kidijitali. Nimejuilishwa kuwa mkutano huu umetoa maazimio mbali mbali ya utekelezaji wa shughuli za kielimu ambayo yamekwenda sambamba na maeneo ya mageuzi. Nina imani kuwa maazimio ya mkutano huu yatafanyiwa kazi kwa haraka na kwa ufanisi. Mageuzi ya elimu si jukumu la Serikali pekee, ni jukumu la kila mdau. Kila taasisi, kila mzazi, kila mwalimu, kila mwanafunzi, na kila mshirika anapaswa kujiona kama sehemu ya suluhisho.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Mwisho kabisa napenda niwashukuru tena washiriki wote kuanzia maandalizi wa mkutano huu mkuu wa pamoja wa tathmini ya elimu, hakika tunathamini michango na maoni yenu muliyotoa na kwakweli yatasaidia sana kuimarisha sekta ya elimu. Mabadiliko katika sekta ya elimu yatafanikiwa iwapo kila mmoja wetu na kila taasisi itatimiza wajibu wake. Serikali itatimiza wajibu wake; na naomba kila mdau atimize wajibu wake.

**Ndugu washiriki na wageni waalikwa**

Heshima niliyopewa ni kwa ajili ya kufunga mkutano huu wa siku tatu, hivyo natumia fursa hii kuendelea kuwaomba Wadau wa Elimu wote waendelee kutuunga mkono kwa sababu ***mageuzi ya elimu hayawezi kusubiri, kila siku ni nafasi mpya ya kujenga mustakabali bora. Tushikamane, tuwajibike, tubadilike – kwa vizazi vya leo na kesho.***

Baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa, natamka rasmi kuwa Mkutano wa Nane wa Tathmini ya Pamoja ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu Zanzibar umefungwa rasmi.

Namuomba mola awarudishe nyumbani salama, mkiwa na ari mpya ya kuchochea mageuzi ya elimu kwa vitendo.

Nawashukuru tena kwa mara nyingine kwa ushiriki wenu mzuri na wenye mafanikio.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**